# BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 27 Februari, 2025.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Wastaafu, Nam. 2 ya 2012 na Kutunga Sheria ya Mafao ya Kustaafu Utumishi wa Kisiasa kwa ajili ya Kuweka Masharti ya Kutoa Mafao na Huduma kwa Viongozi Waliostaafu Utumishi wa Kisiasa na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Wastaafu, Nam. 2 ya 2012 na Kutunga Sheria ya Mafao ya Kustaafu Utumishi wa Kisiasa kwa ajili ya Kuweka Masharti ya Kutoa Mafao na Huduma kwa Viongozi Waliostaafu Utumishi wa Kisiasa na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

133. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    (a) Takwimu ziko vipi juu ya viwango vya uzalishaji wa taka kwa kila mtu nchini mwetu.

    (b) Ni kilogramu ngapi za taka ngumu huzalishwa kwa kila siku kwa Mkoa wa Mjini Magharibi.

    (c) Ni tani ngapi za taka kwa kila siku huzalishwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

134. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Tathmini kwa sasa iko vipi juu ya uwezo wa ukusanyaji wa taka zinazorejewa kutumika tena (reuse, recovery and recycling business).

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

119. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Kwa namna gani mifumo ya teknolojia inaweza kumlinda mtoa taarifa za rushwa ili kuchochea uwajibikaji wa kujenga taifa bora zaidi ifikapo 2050.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

157. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Ugumu wa kupata mikopo kutokana na kutokuwepo kwa uhakika wa marejesho kunawakwaza wakulima wadogo wadogo kujiendeleza vyema.

Je, Serikali inafkiria nini cha kufanya kwa wakulima hawa ili kunufaika na mikopo nafuu kwa azma ya kuwaendeleza kufikia katika malengo yao.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi :**

56. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Ni kwa kiasi gani suala mtambuka la jinsia limepewa mazingatio katika usimamizi wa rasilimali za uchumi wa buluu.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

186. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ujenzi wa skuli nyingi za ghorofa kwa Unguja na Pemba ni moja katika hatua za kuimarisha miundombinu ya kusoma na kusomeshea Zanzibar. Hata hivyo, hakuonekani kuwa na mpango madhubuti wa kuziendesha kwa ufanisi skuli hizo kwa sababu ya kukosekana au kutopelekwa fedha za kutosha za uendeshaji.

(a) Kwa wastani, ni kiasi gani cha fedha kinahitajika kwa mwezi katika uendeshaji wa skuli za ghorofa.

(b) Je, ni athari gani zinapatikana kwa kuziruhusu skuli kukodisha maeneo yake kwa shughuli za kupiga taarabu ili ziweze kumudu gharama za uendeshaji.

(c) Je, ni upi uwezo wa Kamati za Uongozi za Skuli (SMCs) katika kupanga matumizi sahihi ya maeneo ya skuli za ghorofa.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

163. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Je, ni fursa zipi zinapatikana katika uwekezaji wa sekta ya mifugo Zanzibar.

164. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Ni kwa utaratibu gani Wizara yako inawasaidia wafugaji kupata mbegu za mifugo zenye ubora na viwango stahiki.

(b) Kwa kiasi gani mabadiliko ya hali ya hewa yanaathiri ustawi na maendeleo ya sekta ya mifugo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

162. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

(a) Ipi tathmini ya uboreshaji wa miundombinu ya usafiri ili kufikia malengo ya kuwa na mji wa kisasa Zanzibar.

(b) Kwa kiasi gani maji taka yanatumika katika kazi mbali mbali ikiwemo za ujenzi, ili kuyawacha maji safi kutumika katika shughuli za msingi zaidi.

188. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Pamoja na kauli za Serikali za kukusudia kuifungua Pemba kupitia bandari inayoweza kutoa huduma za kimataifa, bado kauli hizo hazijaoana na hali halisi ya bandari za Pemba.

(a) Ni kwa nini hadi sasa bandari za Pemba hazijaweza kufanya kazi kama ilivyoazimiwa.

(b) Ni lini Serikali itapeleka kreni kwa ajili ya kupakuwa makasha (containers) moja kwa moja kwenda kwenye magari (truck).

## <u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

128. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kiasi gani kukuwa, kusambaa na kuenea kwa lugha ya Kiswahili duniani kunachochea ongezeko la uchumi wetu.

129. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Wakati Serikali ikiendelea na ujenzi wa jengo kubwa la Chuo Cha Sanaa, Muziki na Utamaduni, kuna haja ya kufahamu mambo kadhaa ya uimarishaji wa chuo hicho.

(a) Je, Wizara inajiandaa vipi kukabiliana na uhaba wa wakufunzi wabobezi wa tasnia hizi katika chuo hicho.

(b) Ni mikakati gani hasa Serikali inachukua katika kuzalisha wasanii wa maigizo, muziki na sanaa mbali mbali kupitia chuo hicho.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

94. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Pamoja na juhudi mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali za kuwahamasisha wananchi juu ya kutembelea makumbusho ya Zanzibar ili kujifunza mambo mbali mbali ya kihistoria.

Je, takwimu iko vipi juu ya hamasa, uelewa na ongezeko la wananchi katika kutembelea makumbusho hayo.

145. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu mbali mbali imekuwa ikifanya jitihada za kuhifadhi, kulinda na kuutunza Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao ni urithi wa dunia. Pamoja na hayo yapo mambo ambayo yanasababisha msongamano wa vyombo vya moto katika eneo hilo na kuondoa ile haiba ya Mji Mkongwe.

(a) Je, Wizara inalichukulia vipi wazo la kuwa na utaratibu wa kutumia baiskeli kijamaa hususan katika eneo la Mji Mkongwe ili kupunguza msongamano wa vyombo.

(b) Ni yepi matarajio ya ubora wa Jiji la Zanzibar ifikapo mwaka 2050.

**Wizara ya Afya:**

181. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wafanyakazi na madaktari waliohamishwa kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja kwenda Hospitali ya Mkoa ya Lumumba kuhusiana na mishahara midogo na isiyoridhisha huku wakiwa chini ya usimamizi wa wawekezaji badala ya Serikali.

(a) Je, ni upi utaratibu wa usimamizi na maslahi ya madaktari wa Hospitali ya Mkoa ya Lumumba waliotokea Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja.

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani katika kupunguza tofauti kubwa iliyopo ya mishahara na maslahi mengine kati ya madaktari wazawa na wageni wenye sifa zinazofanana.

184. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Zoezi la kubinafsisha huduma za afya Zanzibar bado limeendelea kuwabagua Madaktari Bingwa walioajiriwa na Serikali.

(a) Je, ni upi mpango wa sasa wa Serikali wa kuwa na viwango vinavyoeleweka vya mishahara ya Madaktari Bingwa (Specialists) wa Serikali kama ambavyo Madaktari wa Kampuni Binafsi wanaofanya kazi ya Serikali wanalipwa katika viwango vya Madaktari Bingwa (Specialists).

(b) Je, hadi sasa ni Madaktari Bingwa wangapi wamebaki kama waajiriwa wa Serikaki na wangapi wanaendelea kufanya kazi kupitia Kampuni kwa Unguja na Pemba.

(c) Je, ni utaratibu gani umetumiwa kuwatathimini Madaktari kutoka nje kitaaluma, ujuzi na uzoefu (assessment of knowledge, skill and experience) na kuwapatia leseni za kufanya kazi Zanzibar wakati wengine wanafahamika kwamba ndio kwanza wanajifunza kazi (junior specialists).

<u>**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**</u>

24. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa kiasi gani kuimarika kwa Sekta ya ujenzi katika ujenzi wa miradi mbali mbali ya kimkakati nchini, kunasaidia kukua na kuimarika kwa sekta ya biashara kwa wafanyabishara wa ndani wanaojihusisha na vifaa vya ujenzi.

127. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Wananchi hususani wakulima wa mwani wana matarajio makubwa juu ya uwepo wa kiwanda kikubwa cha kusarifu zao hilo.

(a) Je, mpaka sasa kiwanda hiki kimefikia katika hatua gani.

(b) Kwa kiasi gani kitakuwa na ubora katika suala zima la vifaa na mitambo ya kisasa ya kusarifu zao hilo.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Wastaafu, Nam. 2 ya 2012 na Kutunga Sheria ya Mafao ya Kustaafu Utumishi wa Kisiasa kwa ajili ya Kuweka Masharti ya Kutoa Mafao na Huduma kwa Viongozi Waliostaafu Utumishi wa Kisiasa na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**27 Februari, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**